**MUHTASARI WA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI (KAWAIDA) ULIOFANYIKA TAREHE 30-31/03/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA WILAYA YA MISUNGWI**

**SIKU YA KWANZA TAREHE 30/03/2021**

**WAJUMBE WALIOHUDHURIA.**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Kashinje Machibya Erasto | - | Mwenyekiti wa Halmashauri | |
| 2. | Mhe. Rahma Emmanuel Fidel | - | Makamu Mwenyekiti | |
| 3. | Mhe. Bilarmini H. Kihayile | - | Mjumbe - | Koromije |
| 4. | Mhe. Jogoli K. Mayombo | - | Mjumbe - | Sumbugu |
| 5. | Mhe. Yona Shimbewangoso | - | Mjumbe - | Mamaye |
| 6. | Mhe. Enos Mihayo Nestory | - | Mjumbe - | Gulumungu |
| 7. | Mhe. Fideli Lazaro Kabidi | - | Mjumbe - | Kasololo |
| 8. | Mhe. Ngagizi Makoye Zozozo | - | Mjumbe - | Lubili |
| 9. | Mhe. Faustine Msafiri | - | Mjumbe - | Nhunduru |
| 10. | Mhe. Malale Petro Lutonja | - | Mjumbe - | Mabuki |
| 11. | Mhe. Adelina Mathias | - | Mjumbe - | Buhunda |
| 12. | Mhe. Dotto S. Lugwisha | - | Mjumbe - | Misasi |
| 13. | Mhe. Muganyizi L. Feluzi | - | Mjumbe - | Misungwi |
| 14. | Mhe. Edward R. Dawson | - | Mjumbe - | Idetemya |
| 15. | Mhe. Mathew Mussa Makoye | - | Mjumbe - | Ukiriguru |
| 16. | Mhe. Angela G. Isandiko | - | Mjumbe - | Usagara |
| 17. | Mhe. Kanzaga K. Ezekiel | - | Mjumbe - | Kijima |
| 18. | Mhe. Mayila Simon Maguha | - | Mjumbe - | Shilalo |
| 19. | Mhe. Raphael Athuman Kaboya | - | Mjumbe - | Isenengeja |
| 20. | Mhe. Luzambya Luhweja Simuda | - | Mjumbe - | Buhunda |
| 21. | Mhe. Dome Kazungu Manyasa | - | Mjumbe - | Busongo |
| 22. | Mhe. Monica Nungula Lushiku | - | Mjumbe - | Lubili |
| 23. | Mhe. Marco Lucas Kadala | - | Mjumbe - | Buhingo |
| 24. | Mhe. Ng'wanza M. Nyahehe | - | Mjumbe - | Mwaniko |
| 25. | Mhe. Samson N. Mbizo | - | Mjumbe - | Mondo |
| 26. | Mhe. Amina A. Mwandu | - | Mjumbe - | Mbarika |
| 27. | Mhe. Ruth R. Seni | - | Mjumbe - | Kijima |
| 28. | Mhe. Hindu Yahaya Kimila | - | Mjumbe - | Misungwi |
| 29. | Mhe. Christina L. Nyanda | - | Mjumbe - | Mamaye |
| 30. | Mhe. Beatrice Kabulule | - | Mjumbe - | Usagara |
| 31. | Mhe. Joel Dogani | - | Mjumbe - | Mbarika |
| 32. | Mhe. Bernard D. Polycarp | - | Mjumbe - | Igokelo |
| 33. | Mhe. Paul M. Kishinda | - | Mjumbe - | Fella |
| 34. | Mhe. Daniel M. Busalu | - | Mjumbe - | Misasi |

**WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA - KWA TAARIFA.**

1. Mhe. Jojo Mohamed - Mjumbe - Ilujamate
2. Mhe. Daniel Richard Makoye - Mjumbe - Kanyelele
3. Mhe.Alexander Pastory Mnyeti - Mbunge

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

1. Ndg. Leokadia G. Humera - Katibu - Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)
2. Ndg. Said Ally - Kaimu Afisa Utumishi (W)
3. Ndg. Frederick Nyoka - Afisa Ardhi na Maliasili (W)
4. Ndg. Kwilasa Mahigu - Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W)
5. Ndg. Faustine Salala - Mthibiti Ubora wa shule (W)
6. Ndg. Diana Kuboja - Afisa Elimu Sekondari (W)
7. Ndg. Dickson Kawovela - Kaimu Afisa Uchaguzi (W)
8. Ndg. Bernadetha Sanga - Mratibu UKIMWI (W)
9. Ndg. Upendo Naftali - Afisa Maendeleo ya Jamii (W)
10. Ndg. Stella Msangya - Mweka Hazina (W)
11. Ndg. Sindagulu Jonas - Kaimu Mkaguzi wa ndani (W)
12. Ndg. Mwanajumbe Zuberi - Kaimu Afisa Mipango (W)
13. Ndg. Beatrice Balige - Afisa Elimu Msingi (W)
14. Ndg. Benjamini Salakikya - Kaimu Mhandisi Ujenzi(W)
15. Ndg. Manyanza Mageme - Katibu TSC (W)
16. Ndg. Joseph Nkwabi - Kaimu Afisa TEHAMA (W)
17. Ndg. Thomas Lutego - Afisa Habari (W)
18. Ndg. Zulfa Nuru - Afisa Mapato (W)
19. Ndg. Dorcas Nigha - Kaimu Afisa Nyuki (W)
20. Ndg. Dominic Okoth - Kaimu Afisa Mazingira (W)
21. Ndg. Grolia Buname - Mratibu TASAF (W)
22. Ndg. Juliana Luhasile - Kaimu Afisa Uvuvi(W)
23. Ndg. Cresensia Mwalongo - Afisa Tarafa - Mbarika
24. Dr. Chrispine Shami - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
25. Dr. Clement Morabu - Kaimu Mganga Mkuu (W)
26. Ndg. Prepetua Chonja - Afisa Tarafa – Usagara
27. Ndg. Henry Rumanyika - Kaimu Mwanasheria (W)
28. Ndg. Chrisitina Katole - Afisa Manunuzi (W)
29. Ndg. Peter Michael - Afisa Tarafa- Misungwi

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Martha Mbise
2. Ndg. Bruno Simon
3. Ndg. Deodatus Seleman

## SIKU YA PILI TAREHE 31/3/2021

## WAJUMBE WALIOHUDHURIA

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mhe. Kashinje Machibya Erasto | - | Mwenyekiti wa Halmashauri | - | Usagara |
| 2. Mhe. Rahma Emmanuel Fidel | - | Makamu Mwenyekiti | - | Bulemeji |
| 3. Mhe. Bilarmini H. Kihayil | - | Mjumbe | - | Koromije |
| 4. Mhe. Jogoli K. Mayombo | - | Mjumbe | - | Sumbugu |
| 5. Mhe. Yona Shimbewangoso | - | Mjumbe | - | Mamaye |
| 6. Mhe. Enos Mihayo Nestory | - | Mjumbe | - | Gulumungu |
| 7. Mhe. Fideli Lazaro Kabidi | - | Mjumbe | - | Kasololo |
| 8. Mhe. Ngagizi Makoye Zozozo | - | Mjumbe | - | Lubili |
| 9. Mhe. Faustine Msafiri | - | Mjumbe | - | Nhundulu |
| 10. Mhe. Malale Petro Lutonja | - | Mjumbe | - | Mabuki |
| 11. Mhe. Adelina Mathias | - | Mjumbe | - | Buhunda |
| 12. Mhe. Dotto S. Lugwisha | - | Mjumbe | - | Misasi |
| 13. Mhe. Muganyizi L. Feluzi | - | Mjumbe | - | Misungwi |
| 14. Mhe. Edward R. Dawson | - | Mjumbe | - | Idetemya |
| 15. Mhe. Mathew Mussa Makoye | - | Mjumbe | - | Ukiriguru |
| 16. Mhe. Angela G. Isandiko | - | Mjumbe | - | Usagara |
| 17. Mhe. Kanzaga K. Ezekiel | - | Mjumbe | - | Kijima |
| 18. Mhe. Mayila Simon Maguha | - | Mjumbe | - | Shilalo |
| 19. Mhe. Raphael Athuman Kaboya | - | Mjumbe | - | Isenengeja |
| 20. Mhe. Luzambya Luhweja Simuda | - | Mjumbe | - | Buhunda |
| 21. Mhe. Dome Kazungu Manyasa | - | Mjumbe | - | Busongo |
| 22. Mhe. Monica Nungula Lushiku | - | Mjumbe | - | Lubili |
| 23. Mhe. Marco Lucas Kadala | - | Mjumbe | - | Buhingo |
| 24. Mhe. Ng'wanza M. Nyahehe | - | Mjumbe | - | Mwaniko |
| 25. Mhe. Samson N. Mbizo | - | Mjumbe | - | Mondo |
| 26. Mhe. Amina A. Mwandu | - | Mjumbe | - | Mbarika |
| 27. Mhe. Ruth R Seni | - | Mjumbe | - | Kijima |
| 28. Mhe. Hindu Yahaya Kimila | - | Mjumbe | - | Misungwi |
| 29. Mhe. Christina L. Nyanda | - | Mjumbe | - | Mamaye |
| 30. Mhe. Beatrice Kabulule | - | Mjumbe | - | Usagara |
| 31. Mhe. Joel Dogani | - | Mjumbe | - | Mbarika |
| 32. Mhe. Bernard D. Polycarp | - | Mjumbe | - | Igokelo |
| 33. Mhe. Paul M. Kishinda | - | Mjumbe | - | Fella |
| 34. Mhe. Daniel M. Busalu | - | Mjumbe | - | Misasi |
| 35. Mhe. Jojo Mohamed | - | Mjumbe | - | Ilujamate |
| 36. Mhe. Daniel Richard Makoye | - | Mjumbe | - | Kanyelele |
| 37. Mhe.Alexander Pastory Mnyeti | - | Mbunge | - | Misungwi |

## WAJUMBE AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA

Hakuna

**WAGENI WAALIKWA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg. Gambadu Samweli | - | Mwenyekiti CCM (W) |
| 2. Ndg. Happines Nyamasagala | - | Kaimu Katibu CCM (W) |
| 3. Mhe. Juma Sweda | - | Mkuu wa Wilaya |
| 4. SSP. Shabu B. Shabu | - | Mkuu wa Polisi (W) |
| 5. Ndg. Daniel John | - | Afisa Usalama (W) |
| 6. Ndg. Mathew M. Kilingo | - | Afisa Uhamiaji (W) |
| 7. Ndg. Aisha Mashaka | - | Afisa NIDA |
| 8. SGT. Lushinge PS | - | Kaimu Mshauri wa Mgambo (W) |
| 9. Ndg. George Binagi | - | Mwandishi BLOG |
| 10. Ndg. Swalehe Juma | - | Mwandishi Matukio Daima |
| 11. Ndg. Emmanuel Meshack | - | Mwandishi Dar. mpya TV |
| 12. Ndg. Moses Mathew | - | Mwandishi TBC |
| 13. Ndg. Petro Sabato | - | Katibu Tawala (W) |
| 14. Ndg. Emma Mwasyoge | - | Afisa TAKUKURU |
| 15. Ndg. Frenckson Kanyere | - | Kaimu Meneja RUWASA |
| 16. Eng. Deocatus Chaula | - | Kaimu Meneja TARURA |
| 17. Eng. Wilbert Bujiku | - | Meneja MWAUWASA |
| 18. Ndg. Baraka Chacha | - | Kaimu Meneja TANESCO |

**WATENDAJI WALIOHUDHURIA**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Ndg.Kisena Mabuba | - | Katibu - Mkurugenzi Mtendaji (W) |
| 2. Ndg. Leokadia G. Humera | - | Afisa Utumishi (W) |
| 3. Ndg. Frederick Nyoka | - | Afisa Ardhi na Maliasili (W) |
| 4. Ndg. Kwilasa Mahigu | - | Kaimu Afisa Kilimo na Ushirika (W) |
| 5. Ndg. Faustine Salala | - | Mthibiti Ubora wa shule (W) |
| 6. Ndg. Diana Kuboja | - | Afisa Elimu Sekondari (W) |
| 7. Ndg. Dickson Kawovela | - | Kaimu Afisa Uchaguzi (W) |
| 8. Ndg. Bernadetha Sanga | - | Mratibu UKIMWI (W) |
| 9. Ndg. Upendo Naftali | - | Afisa Maendeleo ya Jamii (W) |
| 10. Ndg. Stella Msangya | - | Mweka Hazina (W) |
| 11. Ndg. Sindagulu Jonas | - | Kaimu Mkaguzi wa ndani (W) |
| 12. Ndg. Mwanajumbe Zuberi | - | Kaimu Afisa Mipango (W) |
| 13. Ndg. Beatrice Balige | - | Afisa Elimu Msingi (W) |
| 14. Ndg. Benjamini Salakikya | - | Kaimu Mwandisi Ujenzi(W) |
| 15. Ndg. Manyanza Mageme | - | Katibu TSC (W) |
| 16. Ndg. Joseph Nkwabi | - | Kaimu Afisa Tehama (W) |
| 17. Ndg. Thomas Lutego | - | Afisa Habari (W) |
| 18. Ndg. Zulfa Nuru | - | Afisa Mapato (W) |
| 19. Ndg. Dorcas Niga | - | Kaimu Afisa Nyuki (W) |
| 20. Ndg. Dominic Okoth | - | Kaimu Afisa Mazingira (W) |
| 21. Ndg. Grolia Buname | - | Mratibu TASAF (W) |
| 22. Ndg. Juliana Luhasile | - | Kaimu Afisa Uvuvi(W) |

23. Ndg. Cresensia Malongo - Afisa Tarafa - Barika
24. Dr. Chrispine Shami - Afisa Mifugo na Uvuvi (W)
25. Dr. Clement Morabu - Kaimu mganga Mkuu (W)
26. Ndg. Prepetua Chonja - Afisa Tarafa - Usagara
27. Ndg. Henry Rumanyika - Kaimu Mwanasheria (W)
28. Ndg. Chrisitina Katole - Afisa Manunuzi (W)
29. Ndg. Peter Michael - Afisa Tarafa- Misungwi

**WATENDAJI AMBAO HAWAKUHUDHURIA KWA TAARIFA**
Hakuna

**SEKRETARIETI**

1. Ndg. Martha Mbise
4. Ndg. Bruno Simon
5. Ndg. Deodatus Seleman

**MUHT. NA. 8/3/2021 KUFUNGUA MKUTANO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue Mkutano kwa vile akidi ya wajumbe ilitimia. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe pamoja na watendaji kwenye mkutano na kuwapa pole kwa msiba uliotokea tarehe 17/3/2021 wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Pia aliwapongeza wajumbe kwa kuwahi kwenye mkutano. Alifungua Mkutano saa 5.08 asubuhi.

**MUHT. NA. 09/03/2021 KUTHIBITISHA AGENDA.**

Agenda zilizokuwa zimeandaliwa ni 13 na wajumbe walikubali kuzijadili kama ifuatavyo:-

1. Kufungua Mkutano.
2. Kuthibitisha agenda
3. Kupokea taarifa za maendeleo ya Kata kutoka kwa Wahe. Madiwani.
4. Kuahirisha Mkutano

**SIKU YA PILI TAREHE 31/3/2021**

5. Kupokea na kujibu maswali ya papo kwa papo.
6. Kupokea salaamu Mbalimbali.
7. Kusoma na kuthibitisha Mihtasari
    (i) Mkutano wa Kawaida tarehe 5-6/5/2020 Robo ya Kwanza.
    (ii) Mkutano Baraza la kwanza tarehe 17/2/2020

(iii) Mkutano Baraza Maalumu Rasimu ya mapendekezo kugawa wilaya mpya ya Kisesa tarehe 28/01/2021
(iv) Mkutno Maalumu Bajeti tarehe 11-12/02/2021

8. Maagizo ya Baraza la Madiwani la tarehe 5-6/05/2020.
9. Kupokea taarifa kutoka kwa wenyeviti wa Kamati za kudumu.
   (i) Kamati ya Udhibiti UKIMWI
   (ii) Kamati ya Masuala ya Kiuchumi
   (iii) Kamati ya Huduma za Kijamii
   (iv) Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango.
10. Kupokea taarifa kutoka Taasisi mbalimbali
   (i) RUWASA
   (ii) MWAUWASA
   (iii) TARURA
   (iv) TANESCO
11. Kupokea taarifa kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya.
12. Masuala ya Kiutumishi
13. Kufunga Mkutano.

**MUHT. NA. 10/3/2021 KUPOKEA TAARIFA ZA MAENDELEO YA KATA KUTOKA KWA WAHE. MADIWANI.**

Mwenyekiti aliwakaribisha Wahe. Madiwani kuwasilisha taarifa za shughuli za maendeleo zilizotekelezwa kwenye kata zao kwa kipindi cha robo ya pili. Taarifa ziliwasilishwa kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Kata ya Mbarika | - | Miradi 8 taarifa ilipokelewa |
| 2. Kata ya Busongo | - | Miradi 3 taarifa ilipokelewa |
| 3. Kata ya Buhunda | - | Miradi 6 taarifa ilipokelewa |
| 4. Kata ya Mwaniko | - | Miradi 4 taarifa ilipokelewa |
| 5. Kata ya Mondo | - | Miradi 2 taarifa ilipokelewa |
| 6. Kata ya Sumbugu | - | Miradi 10 taarifa ilipokelewa |
| 7. Kata ya Buhingo | - | Miradi 5 taarifa ilipokelewa |
| 8. Kata ya Nhundulu | - | Miradi 5 taarifa ilipokelewa |
| 9. Kata ya Isenengeja | - | Miradi 7 taarifa ilipokelewa |
| 10. Kata ya Usagara | - | Miradi 9 taarifa ilipokelewa |
| 11. Kata ya Kijima | - | Miradi 3 taarifa ilipokelewa |
| 12. Kata ya Fela | - | Miradi 4 taarifa ilipokelewa |
| 13. Kata ya Ukiriguru | - | Miradi 6 taarifa ilipokelewa |
| 14. Kata ya Gulumungu | - | Miradi 4 taarifa ilipokelewa |
| 15. Kata ya Kasololo | - | Miradi 6 taarifa ilipokelewa |
| 16. Kata ya Koromije | - | Miradi 8 taarifa ilipokelewa |
| 17. Kata ya Mabuki | - | Miradi 6 taarifa ilipokelewa |
| 18. Kata ya Kanyelele | - | Miradi 5 taarifa ilipokelewa |

19. Kata ya Mamaye - Miradi 9 taarifa ilipokelewa
20. Kata ya Ilujamate - Miradi 6 taarifa ilipokelewa
21. Kata ya Misasi - Miradi 6 taarifa ilipokelewa
22. Kata ya Lubili - Miradi 3 taarifa ilipokelewa
23. Kata ya Shilalo - Miradi 4 taarifa ilipokelewa
24. Kata ya Idetemya - Miradi 4 taarifa ilipokelewa
25. Kata ya Bulemeji - Miradi 5 taarifa ilipokelewa
26. Kata ya Igokelo - Miradi 9 taarifa ilipokelewa
27. Kata ya Misungwi - Miradi 4 taarifa ilipokelewa.

Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa jinsi walivyowasilisha taarifa za Kata, walifanya marekebisho mbalimbali kisha aliwakaribisha kutoa maoni ya jumla kuhusu uwasilishaji wa taarifa hizo.

Wajumbe walishauri kwamba watendaji wa kata pamoja na ofisi ya Mipango wawe wanaandaa taarifa kwa usahihi ili kuondoa Malalamiko.
Mjumbe mwingine alishauri kuwa changamoto zinazotolewa kwenye taarifa ziwe zinatatuliwa pia wajumbe walishauri kuwa Watendaji wa kata wawe wanahudhuria kwenye mkutano na wahe. Madiwani kwa ajili ya kuwasilisha taarifa za kata.

**MUHT. NA.11/ 03/2021 KUAHIRISHA MKUTANO**
Katibu aliwashukuru wajumbe kwa maoni yao, alieleza kuwa suala la Wahe. Madiwani kuhudhuria na Watendaji wa Kata kwenye mkutano litafanyiwa. Alimkaribisha Mwenyekiti ili ahairishe mkutano.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango na maoni yao kisha alisisitiza kwamba:-

(i) Taarifa zinazoandaliwa na Watendaji wa Kata ziwe zinaandaliwa kwa umakini na ufanisi.
(ii) Watendaji wa Kata/Vijiji wawe wanasoma taarifa za mapato na matumizi katika maeneo yao.
(iii) Changamoto zinazoainishwa kwenye taarifa ziwe zinatatuliwa. Aidha aliwatangazia wajumbe kuendelea kusaini kitabu cha Maombolezo kwa Mkuu wa Wilaya kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi,2021. Aliahirisha mkutano saa 6:28 mchana.

**SIKU YA PILI TAREHE 31/03/2021**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya mwendelezo wa mkutano kwa siku ya pili. Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe na watendaji pamoja na wageni waalikwa. Alifungua mkutano saa 5:17 asubuhi.

**MUHT. NA 12/ 3/2021 KUPOKEA NA KUJIBU MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Hapakuwa na maswali ya papo kwa papo yaliyokuwa yameandaliwa.

**MUHT. NA 13/3/2021 KUPOKEA SALAAM MBALIMBALI**

Mwenyekiti aliwakaribisha viongozi waliokuwepo kwenye mkutano watoe salaam zao.

**(i) MWENYEKITI WA CCM.**

Alisisitiza kwamba, pamoja na kuwa katika maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli shughuli za maendeleo ya wananchi ziendelee. Aidha alisisitiza miradi ya maji itekelezwe kwa kiwango cha kuridhisha.

**(ii) MHE. MBUNGE**

Alitoa pole kwa wajumbe na Watendaji na wageni waalikwa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati Dkt. John Pombe Magufuli. Aidha, alisisitiza upendo na kuthaminiana wajumbe ili Halmashauri ya Misungwi iweze kusonga mbele.

**(iii) MHE. MKUU WA WILAYA**

Alieleza kuwa Baraza la Madiwani lipo na linaendeshwa kwa mujibu wa sheria na sio utashi wa mtu. Alisema, kutokana na wahe. Madiwani kutokula chakula siku ya mkutano wa Chama tarehe 29/03/2021 pamoja na siku ya kwanza ya mkutano wa Baraza la Madiwani tarehe 30/3/2021. Mhe. Mkuu wa Wilaya aliagiza kuwa chakula kisiagizwe tena kwenye vikao vya Wahe. Madiwani. Aliwasihi Wahe. Madiwani washiriki ipasavyo kutekeleza miradi ya maji ambayo haijakamilika.

Aliipongeza Wilaya ya Misungwi katika suala zima la elimu kuwa Wilaya imefanya vizuri, matokeo ya Wanafunzi wa Kidato cha Nne mwaka 2020 yanaridhisha.Wanafunzi waliofaulu kwa daraja la I ni zaidi ya 200.

Aidha, alisisitiza wajumbe waendelee kuwahamasisha wananchi kulima zao la Dengu na Choroko. Hata hivyo, aliwasihi TANESCO kata ambazo hazina umeme yaani shilalo, Isenengeja na Lubili ziunganishiwe umeme. Vilevile aliwasihi TARURA wakarabati barabara za vijijini ikiwemo barabara ya Mahando kwa kuwa haipitiki.

**MUHT. NA.14/3/2021 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MIHTASARI YA BARAZA LA MADIWANI.**

**(i) MUHTASARI WA TAREHE 5-6/05/2020 – MKUTANO WA KAWAIDA**

Muhtasari uliwasilishwa mbele ya wajumbe na wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa, waliuthibitisha kuwa ni sahihi hivyo, Mwenyekiti na Katibu waliusaini kuwa kumbukumbu sahihi ya Mkutano.

**(ii) MUHTASARI WA TAREHE 17/12/2020 - MKUTANO BARAZA LA KWANZA.**

Muhtasari uliwasilishwa mbele ya wajumbe na wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa, walithibitisha kuwa ni sahihi hivyo Mwenyekiti na Katibu waliusaini kuwa kumbukumbu sahihi ya Mkutano.

**(iii) MUHTASARI WA TAREHE 28/01/2021 – MKUTANO MAALUM RASIMU YA MAPENDEKEZO YA KUANZISHA WILAYA MPYA YA KISESA.**

Muhtasari uliwasilishwa mbele ya wajumbe na wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa, walithibitisha kuwa ni sahihi hivyo Mwenyekiti na Katibu waliusaini kuwa kumbukumbu sahihi ya Mkutano.

**(iv) MUHTASARI WA TAREHE 11-12/02/2021 – MKUTANO MAALUM BAJETI**

Muhtasari uliwasilishwa mbele ya wajumbe na wajumbe waliupitia ukurasa kwa ukurasa, walithibitisha kuwa ni sahihi hivyo Mwenyekiti na Katibu waliusaini kuwa kumbukumbu sahihi ya Mkutano.

**MUHT. NA. 15/3/2021 MAAGIZO YA BARAZA LA MADIWANI LA TAREHE 5-6/05/2021**

Menejimenti iliwasilisha utekelezaji wa maagizo ya Baraza la Madiwani kama ifuatavyo:-

**(i) Kuhusu wafadhili waliojenga mradi wa wodi ya Wazazi kituo cha Afya Mbarika, na mradi wa ujenzi wa maabara shule ya Sekondari Idetemya waandikiwe barua ya pongezi kwa kazi nzuri waliyofanya.**

Ilijibiwa kuwa wafadhili hao walipewa barua za pongezi ambao ni Field Manager Mama na Mtoto Project, University of Calgaly – Canada na ASAP.

**MUHT. NA.16/3/2021 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU.**

Katibu alitoa hoja kwa Mwenyekiti kwa ajili ya wenyeviti wa Kamati kuwasilisha taarifa kwa kipindi cha robo ya pili. Mwenyekiti aliwaomba wenyeviti kuwasilisha taarifa za Kamati na wenyeviti waliwasilisha taarifa kama ifuatavyo:-

**KAMATI YA UDHIBITI UKIMWI**

Mwenyekiti wa Kamati ya Udhibiti UKIMWI aliwasilisha taarifa ya vikao viwili vilivyofanyika tarehe 18/1/2021 maalum cha Bajeti na tarehe 1/3/2021 kikao cha kawaida na Mihtasari yote ilithibitishwa.

Wajumbe walipitia majadiliano yaliyofanyika pamoja na utekelezaji, walikubaliana iwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI**

Alisema katika kutekeleza mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Halmashauri ilipanga kutumia kiasi cha Tsh. 275,421,000/= kwa ajili ya shughuli za mapambano dhidi ya UKIMWI, kati ya fedha hizo Tsh. 273,421,000/= ni fedha toka mradi wa AGPAHI unaotekelezwa chini ya Idara ya Afya na Tsh. 2,000,000/= toka Halmashauri ya Wilaya (Mapato ya ndani) kwa shughuli zinaozotekelezwa katika jamii kupitia Idara ya maendeleo ya Jamii. Taarifa ilipokelewa.

**TAARIFA YA KAMATI YA MASUALA YA UCHUMI, UJENZI NA MAZINGIRA**

Mwenyekiti wa Kamati ya masuala ya Uchumi, ujenzi na Mazingira aliwasilisha taarifa ya Kamati kwa robo ya pili kwamba kwa kipindi hicho vilifanyika vikao viwili tarehe 20/1/2021 kikao maalum bajeti na tarehe 3/3/2021 kikao cha kawaida. Mihtasari yote ilikuwa imethibitishwa wajumbe walipitia majadiliano yaliyofanyika pamoja na utekelezaji, walikubaliana iwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI**

Alisema katika kutekeleza mpango wa maendeleo kwa mwaka 2020/2021, Halmashauri ilipanga kutumia jumla ya Tsh. 4,844,523,291/= na ilikuwa imepokea Tsh. 121,620,519.56 sawa na asilimia 2.5 ya fedha zilizopangwa. Hadi kuishia tarehe 31/12/2020 Halmashauri ilikuwa imetumia kiasi cha Tsh. 119,620,519.56 sawa na asilimia 98.4 ya fedha pokelewa kwa mchanganuo ufuatao:-

| Na. | Jina la Mradi | Fedha pangwa | Fedha tolewa | Fedha tumika |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Miradi ya Mapato ya Ndani (40%) | 516,266,250 | 106,755,519.56 | 106,755,519.56 |
| 2. | Mfuko wa Jimbo (CDCF) | 2,000,000 | 2,000,000.00 | 0 |
| 3. | Ukamilishaji wa Jengo la Ofisi za Halmashauri | 750,000,000 | 0 | 0 |
| 4. | TASAF | 3,576,257,041 | 12,865,000.00 | 12,865,000.00 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla kuu** | **4,844,523,291** | **121,620,519.56** | **119,620,519.56** |

Aidha aliwasilisha fedha za Bakaa 2019/2020 kuishia 31, Desemba 2020 kama ifuatavyo:-

| Na. | Jina la Mradi | Fedha zilizokuwa zimebaki | Fedha tumika kwa mwezi |
|---|---|---|---|
| 1. | TASAF | 33,794,452,.67 | 8,439,300.00 |
| | **Jumla kuu** | **33,794,452,.67** | **8,439,300.00** |

Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia, Mjumbe alihoji kuhusu mradi wa Josho la Fella kuwa ni lini utakamilika.

Afisa Mifugo alijibu kuwa ukamilishaji wa mradi huo unaendelea, zimepungua 'pipe' 8 hivyo, aliomba kupewa fedha ili zitumike kununulia 'pipe' hizo.

Mwenyekiti alisema kwamba, agizo la Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango lizingatiwe kwamba ukamilishaji wa mradi ufanyike kwa gharama zao wenyewe wasimamizi wa mradi huo.

Katibu alieleza kuwa kuhusiana na suala la Josho katika kijiji cha Fella zilishachukuliwa hatua za kuwaandikia barua kuzuia pesa zisitoke kwenye akaunti. Suala hili linatekelezwa na Mkuu wa Idara ya Mifugo na Mhandisi wa Ujenzi msimamizi wa mradi huo hivyo wapo wanatekeleza.
**AGIZO:** Ukamilishaji wa Ujenzi wa Josho katika kijiji cha Fella uendelee kwa gharama za wasimamizi wa mradi huo.

**KAMATI YA HUDUMA ZA KIJAMII.**
Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Kijamii aliwasilisha taarifa ya vikao viwili, tarehe 19/01/2021 maalum bajeti na tarehe 02/03/2021 kikao cha kawaida. Mihtasari ilikuwa imethibitishwa.
Wajumbe walipitia majadiliano yaliyofanyika pamoja na utekelezaji uliofanyika. Walikubaliana iwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

**UTEKELEZAJI WA MIRADI.**
Alisema katika kutekeleza mpango wa maendeleo kwa mwaka 2020/2021 kwa kipindi cha mwezi Disemba 2020 Halmashauri ilikuwa imepokea kiasi cha Tshs. 256,257,270.72 sawa na asilimia 3.9 ya fedha zilizopangwa kwa mwaka mzima ambazo ni Tshs. 6,569,714,330/= Hadi kuishia tarehe 31/12/2020 Halmashauri ilikuwa imetumia kiasi cha Tsh. 165,212,470.39 sawa na asilimia 64.5 ya fedha pokelewa kama ifuatavyo:-

| Na. | Jina la Mradi | Fedha pangwa | Fedha tolewa | Fedha tumika |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Miradi ya Mapato ya ndani (40%) | 186,772,750 | 23,553,000.00 | 23,553,000.00 |
| 2 | Mfuko wa Jimbo (CDCF) | 65,524,000 | 65,524,000.00 | 0 |
| 3 | Health Sector Basket Fend (HSBF) | 802,861,000 | 0 | 0 |
| 4 | RBF | 1,763,928,000 | 0 | 0 |
| 5 | Ukamilishjai wa Zahanati | 150,000,000 | 0 | 0 |
| 6 | Ukamilishaji wa Vyumba vya madarasa shule za Msingi | 125,019,080 | 0 | 0 |
| 7 | Ukamilishaji wa Vyumba vya Maabara katika Shule za Sekondari | 210,000,000 | 0 | 0 |
| 8 | EP4R - Msingi | 200,000,000 | 0 | 0 |
| 9 | EP4R - Sekondari | 200,000,000 | 0 | 0 |
| 10 | LANES | 100,000,000 | 0 | 0 |
| 11 | Benki ya Dunia - (SWASH) | 289,800,000 | 0 | 0 |
| 12 | Benki ya Dunia - (WASH) | 220,000,000 | 0 | 0 |
| 13 | TAHEA | 45,000,000 | 0 | 0 |
| 14 | AGPAH | 273,421,000 | 0 | 0 |
| 15 | Lishe Kimataifa | 15,933,000 | 23,799,641.00 | 0 |
| 16 | Global Fund | 7,525,000 | 7,401,159.33 | 5,680,000.00 |
| 17 | Elimu bila malipo - Msingi | 1,236,933,000 | 90,746,818.58 | 90,746,818.58 |
| 18 | Elimu bila malipo - Sekondari | 676,997,500 | 45,232,651.81 | 45,232,651.81 |
| | **JUMLA KUU** | **6,569,714,330** | **256,257,270.72** | **165,212,470.39** |

Aidha aliwasilisha fedha za Bakaa 2019/2020 kuishia 31 Disemba 2020 kama ifuatavyo:-

| Na. | Jina la Mradi | Fedha iliyokuwa imebaki | Fedha tumika mwezi Disemba |
|---|---|---|---|
| 1 | RBF | 132,703,618.00 | 16,680,546.00 |
| 2 | Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya | 346,100,000.00 | 82,048,940.00 |
| | **Jumla Kuu** | **478,803,618.00** | **98,729,486.00** |

Wajumbe walipokea taarifa na kuchangia:- Mjumbe alihoji ni wagonjwa gani waliopuuzwa?

Kaimu Mganga Mkuu alijibu kuwa wagonjwa waliopuuzwa ni wagonjwa ambao wanakuja hospitali na wanaachwa na ndugu zao, hivyo Serikali huwa inawahudumia wakipona wanarudishwa kwao.

Mjumbe mwingine alieleza kuwa huduma inayotolewa katika hospitali ya wilaya ni hafifu.
Katibu alieleza kuwa Kaimu Mganga Mkuu atafuatilia suala hilo na ataliwasilisha kwenye kikao cha Bodi ili huduma ziweze kuboreshwa.

**KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO**

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya fedha, Uongozi na Mipango aliwasilisha taarifa ya vikao vitatu tarehe 21/01/2021 Kikao Maalum Bajeti, tarehe 27/01/2021 Kikao Maalum kujadili Rasimu ya mapendekezo ya kuunda wilaya mpya ya Kisesa na tarehe 05/03/2021 kikao cha kawaida. Mihtasari yote ilikuwa imethibitishwa, pia kamati ilikuwa imefanya ziara ya ukaguzi wa miradi tarehe 04/03/2021.
Wajumbe walipokea agenda zilizojadiliwa pamoja na utekelezaji wa maagizo walikubaliana iwe kumbukumbu sahihi ya Halmashauri.

Aidha aliwasilisha taarifa ya Mapato na Matumizi kuishia Mwezi Disemba 2020 kama ifuatavyo:-

**A. MAPATO**

**i. MAPATO KUTOKANA NA VYANZO VYA NDANI.**

Halmashauri ilikisia kukusanya Tshs. 2,300,000,000/= kwa bajeti ya mwaka 2020/2021 hadi kufikia Mwezi Disemba, 2020 jumla ya Tshs. 1,199,664,966.46 zilikuwa zimekusanywa sawa na asilimia 52.16.

**ii. MAPATO KUTOKANA NA RUZUKU YA MATUMIZI MENGINEYO (OC).**

Halmashauri ilikisia kupokea Tshs. 1,374,229,400/= kama ruzuku ya matumizi mengineyo kwa mwezi Disemba 2020 zilipokelewa jumla ya Tshs. 881,366,500/= sawa na asilimia 64.14.

**iii. MAPATO KUTOKANA NA RUZUKU YA MISHAHARA (PE).**

Halmashauri ilikisia kupokea Tshs. 29,676,478,591/= kama ruzuku ya Mishahara, hadi kufikia mwezi Disemba 2020 zilipokelewa jumla ya Tshs. 14,181,346,430/= sawa na asilimia 47.7.

**iv. MAPATO KUTOKANA NA RUZUKU YA MAENDELEO.**

Halmashauri ilikisia kupokea Tshs. 7,110,325,632/= kama ruzuku ya Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia Mwezi Disemba, 2020 jumla ya Tshs. 1,306,593,470.44 zilipokelewa sawa na asilima 18.38.

**B. MATUMIZI.**

**i. MATUMIZI KUTOKANA NA VYANZO VYA NDANI**

Hadi kufikia Mwezi Disemba 2020, jumla ya Tshs. 436,788,714.19/= zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 45.89.

### ii. MATUMIZI MENGINEYO (OC)

Hadi kufikia Mwezi Disemba 2020, jumla ya Tshs. 771,299,050.88 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 56.13.

### iii. MATUMIZI YA MISHAHARA.

Hadi kufikia Mwezi Disemba 2020, jumla ya Tshs. 14,181,346,430/= zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 47.79.

### iv. MATUMIZI YA MIRADI YA MAENDELEO.

Hadi kufikia Mwezi Disemba 2020, jumla ya Tshs. 446,782,251.61 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 49.27.

Baada ya taarifa kuwasilishwa Wajumbe walipokea na kuchangia:-

Mjumbe alihoji kuhusu Kampuni ya CCECC inayojenga daraja Kigongo Ferry itatoa lini fedha kiasi cha Tshs. 50,000,000/= kama fidia ya eneo la mlima wa kijiji zinako sagwa kokoto.

Mwekahazina alijibu kwamba, Kampuni ya CCECC itaandikiwa barua kuitaka ifikapo tarehe 30 Juni, 2021 iwe imelipa fedha hizo kama fidia.

## MUHT. NA.17/3/2021 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA TAASISI MBALIMBALI.

### 1. RUWASA.

Meneja RUWASA aliomba radhi kwa kuwa taarifa yake ilikuwa haijaandaliwa.

**AGIZO:** Iwasilishwe taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Taasisi ya RUWASA kipindi cha Robo ya Pili 2020/2021 katika Mkutano ujao

### 2. MWAUWASA.

Meneja MWAUWASA aliwasilisha taarifa ya utekelezaji Robo ya pili 2020/2021 kwamba:-

i) MWAUWASA inatoa huduma ya maji safi katika mji wa Misungwi kwa kata ya Misungwi na Igokelo.

ii) Mamlaka imeendelea kupambana na upotevu wa maji na kufanikiwa kupunguza maji yanayopotea kutoka asilimia 40, mwaka uliopita hadi kufikia asilimia 26 Mwezi Disemba, 2020.

iii) Wateja 3,382 wanaohudumiwa na Mamlaka wamefungiwa dira za maji.

Aliwasilisha gharama za uzalishaji maji katika kipindi cha robo ya pili kama ifuatavyo:-

| Mwezi | Gharama ya Umeme | Gharama ya Dawa | Jumla |
|---|---|---|---|
| Oktoba | 14,935,608.59 | 3,215,400.00 | 18,151,008.59 |
| Novemba | 10,890,919.26 | 3,531,300.00 | 14,422,219.26 |
| Disemba | 12,277,480.98 | 3,569,400.00 | 15,846,880.98 |
| **Jumla** | **38,104,008.83** | **10,316,100.00** | **48,420,108.83** |

Aidha aliwasilisha mauzo na makusanyo kama ifuatavyo:-

| Mwezi | Maji yaliyouzwa | Fedha iliyokusanywa |
|---|---|---|
| Oktoba | 37,887,100.00 | 42,032,391.69 |
| Novemba | 37,477,750.00 | 43,257,187.00 |
| Disemba | 37,703,506.00 | 40,898,673.36 |
| **Jumla** | **113,068,350.00** | **126,188,252.05** |

Wajumbe walipokea taarifa na uchangia:-
Mjumbe alihoji kuhusu mikakati iliyopo kuhudumia wateja waliopo mbali na zaidi ya Mita 60 kutoka katika chanzo cha Maji.
Meneja MWAUWASA alijibu kwamba wanaendelea kuhudumia wateja kwa zaidi ya Mita 60 lakini gharama za kuunganishiwa huduma zitaongezeka.

Mjumbe mwingine alitaka kujua kuwa kijiji cha Usagara kinahudumiwa na Mamlaka gani ya maji,hivyo aliomba kijiji cha Usagara kipelekewe maji.
Meneja MWAUWASA alijibu kuwa Usagara ipo chini ya RUWASA lakini mradi mkubwa uliosanifiwa upo chini ya MWAUWASA na ukikamilika Usagara I ytakuwa chini ya MWAUWASA.

3. **TARURA.**

Meneja wa TARURA aliwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za Barabara kupitia TARURA katika kipindi kinachoishia tarehe 28 Februari, 2021 mwaka 2020/2021 kwamba katika mwaka wa fedha 2020/2021 wilaya ya Misungwi kupitia TARURA ilitengewa kiasi cha Tshs. 1,773,008,519.49 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za barabara, kati yake kiasi cha Tshs. 834,621,149.47 ni kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kawaida wa ukarabati wa Barabara na kiasi cha Tshs. 938,387,370/= ni kwa ajili ya mpango wa Maendeleo.

Hadi tarehe 16 Machi, 2021 Halmashauri ya Misungwi ilikuwa imepokea jumla ya Tshs. 973,421,603.47 ambapo Tshs. 439,779,202.47 ni fedha za ukarabati wa Barabara (Road Maintenance) na Tshs. 533,633,401/= fedha za Maendeleo (Development Projects) za ujenzi wa daraja la Mwasonge pamoja na ujenzi wa Barabara za Misungwi mjini Km 1 kwa kiwango cha Lami.
Pamoja na mpango huu, Halmashauri ya Misungwi inakamilisha utekelezaji wa kazi zilizovuka mwaka amabapo Mkataba mmoja (1) unatekelezwa ambao ni AE/092/2019 – 2020/MZA/W/55 wenye gharama ya Tshs. 481,777,860.00

Pia aliwasilisha utekelezaji wa jumla ya miradi 7 ya 2019/2020 na 2020/2021 mpaka tarehe 16 Machi,2021 ambayo iko katika hatua mbalimbali.
Aidha alisema, Ofisi ya TARURA ilipangiwa kutumia kiasi cha Tsh.791,580,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa barabara za Wilaya za jumla ya KM 112katika ukomo elekezi uliotolewa ambao ni sawa na asilimia 12 ya barabara zilizosajiliwa za jumla ya KM927.54

Kama ifuatavyo:-

A. MATENGENEZO YA KAWAIDA.

i. Barabara ya Misungwi - Nange Km 10.
ii. Barabara ya Misungwi - Township Km 10.
iii. Barabara ya Misungwi - Mondo Km 10.
iv. Barabara ya Mbarika - Ilujamate - Mwawile Km 10.
v. Barabra ya Manawa - Kasololo - Mbarika Km 10.
vi. Barabara ya Seeke - Gulumungu - Nyambiti Km 7.
vii. Barabara ya Mondo - Mwaniko - Lubuga Km 8.
viii. Barabara ya Misungwi - Koromije Km 6.

B. MATENGENEZO YA MAENEO KOROFI.

i. Mwagiligili - Mwamagili - Kwimba Border Km 6.
ii. Maganzo - Kwimba Border Km 3.
iii. Buhunda - Isesa Km 3.
iv. Mbarika - Ilujamate - Mwawile Km 5.
v. Manawa - Kasololo - Mbarika Km 8.
vi. Seeke - Gulumungu - Nyambiti Km 3.
vii. Mondo - Mwaniko - Lubuga Km 2.
viii. Usagara Township Km 5.

C. MATENGENEZO MAALUM.

i. Misungwi Township Km4.
ii. Usagara Township Km 1.
iii. Mnadani - Old Tanroad Km 1.
iv. Madaraja - Misungwi Township.
v. Madaraja - Kuimba Boarder.
vi. Buhunda - Isesa.
vii. Seeke - Gulumungu - Nyambiti.
viii. Manawa - Kasololo - Mbarika.

Baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipokea na kupendekeza barabara zifuatavyo zitengenezwe kama ifuatavyo:-

i. Barabara ya Kasololo kwenda kwenye Zahanati ya Nyamijundu.
ii. Barabara ya Myamle kwenda Mwagala.
iii. Barabara ya Isenengeja kwenda Mahando.
iv. Barabara ya Misungwi - Mondo - iwekewe karavati.
v. Barabara ya Ndinga - Mwaniko - iwekewe karavati.

**4. TANESCO.**

Taarifa ilikuwa haijaandaliwa kwa maandishi hivyo, wajumbe waliagiza iwasilishwe kwenye mkutano ujao kwa maandishi.

**MUHT.N.17/3/2021 KUPOKEA TAARIFA KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**I. VITAMBULISHO VYA WAJASILIAMALI**

Mkurugenzi Mtendaji(W) alitoa taarifa kuwa Halmshauri ya Wilaya Misungwi imepokea vitambulisho 7,000 vya wajasiliamali ambapo watendaji wa kata/vijiji watahusika kuvigawa kwa wajasiliamali.

**II. KODI ZA MAJENGO**

Mkurugenzi Mtendaji (W) alitoa taarifa kuhusiana na kodi za majengo
kwamba maelekezo ya serikali ya awali ilikuwa nyumba zote za mabati katika Wilaya ndizo zitakazosajiliwa na kutozwa kodi ya majengo lakini kwa sasa maeneo ya kata ya Misungwi na Usagara ndio yatakayotozwa kodi ya majengo peke yake.

**III. UMALIZIAJI WA UJENZI WA ZAHANATI**

Mkurugenzi Mtendaji(W) alitoa taarifa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi imepokea fedha za umaliziaji wa ujenzi wa zahanati katika Wilaya ya Misungwi na tayari zimepelekwa kwenye miradi husika,aliwasihi wahe. Madiwani washiriki kusimamia miradi hiyo.

**MUHT.NA.18/3/2021 MASUALA YA KIUTUMISHI**

Afisa Utumishi kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya aliwasilisha taarifa ya masuala ya kiutumishi kama ifuatavyo:-
Aliwasilisha mapendekezo ya watumishi kumi na mbili (12) ili wathibitishwe kazini ambao ni:-

1. Everius Pontian Jeremiah
2. Sosoma God Kibinza
3. Edwin Rono Chobosi
4. Robert Nkuba Mashimo
5. Water Deo Mtaki
6. Ackilina Mathias Zacharia
7. Noel Charles Kitwe
8. Mihigo William Nabehu
9. Godfrey Faustine Zengo
10. Mashiri Mathias Mbizo
11. Deusdedith Filbetus Katabalo
12. Francisco Justine Majige

Pia aliwasilisha Mapendekezo ya kumthibitisha mtumishi katika cheo cha ukuu wa Idara baada ya kutimiza miezi 6 katika cheo hicho ambaye ni Ndg. Anna Lazaro Urio
Aidha, aliwasilisha mapendekezo ya kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi 13 wenye tuhuma mbalimbali.

Baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliipokea na waliridhia kuwa watumishi 12 waliopendekezwa kuthibitishwa kazini wathibitishwe kazini na mtumishi aliyependekezwa kuthibitishwa cheo athibitishwe. Aidha, watumishi 13 waliopendekezwa kuchukuliwa hatua za kinidhamu kati yao watumishi 11 hatua za kinidhamu ziendelee na watumishi 2 waliotuhumiwa kwa kosa la kutoa taarifa za uongo kuwa wana vyeti vya kidato cha Nne waitwe kwa Mkurugenzi Mtendaji(W) ili wasikilizwe.

**MUHT.NA.19/3/2021 KUFUNGA MKUTANO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge mkutano kwa vile agenda zote zilikuwa zimejadiliwa.Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe pamoja na watendaji kwa ujumla kisha alifunga mkutano saa 12.18 jioni.

**UMETHIBITISHWA**

| | |
|---|---|
| ............................ | ............................ |
| **KATIBU** | **MWENYEKITI** |
| TAREHE......28/05/2021 | TAREHE......28/05/2021. |